

Najua ABCCh ~ I know the ABC

Hatua ya Pili - Level 2



A B CH D E F G H I J K L M N O P R S T U V W Y Z

Aa



a e i o u

A-Asali-Dada yangu anapenda asali

A-Andazi-Kaka anakula andazi

A-Acha Acha kucheza na maji

A-Afrika- Afrika ina nchi nyingi

A-Andika-Andika herufi Aa

My sister likes honey


Brother is eating doughnuts

Stop playing with water

Africa has many countries

Write the letter Aa

Bb



ba be bi bo bu

Ba-Barakoa -Shangazi ana barakoa nyeupe

Be-Bendera-Bendera ya Canada inapepea

Bi -Birika- Bibi ana birika jeusi

Bo-Boti- Babu ana boti jeupe

Bu-Bundi-Bundi ana pua nyeusi

Aunt has a white mask


The Canada flag is waving

Grandma has a black kettle

Grandpa has a white boat

An owl has a black nose

Ch



cha che chi cho chu

Cha-Chapati-Mama anakula chapati

Che-Chenza-Chenza ni tamu sana

Chi -China-China kuna chakula kitamu

Cho-Choo-Choo chetu kina rangi nyeusi

Chu-Chura -Chura anaruka juu

Mom is eating chapati

Tangerine is very yummy

There is tasty food in China

Our toilet is painted black

The frog jumps up

Dd



da de di do du

Da-Dada-Dada yangu anapenda kula dagaa

De-Dereva-Dereva amefunga mkanda

Di- Dirisha- Mwalimu amefungua dirisha

Do-Dodoma- Dodoma ni mji wa Tanzania

Du-Duara-Mtoto anachora duara

My sister likes to eat sardines

The driver has fasten his seatbelt

The teacher has opened the window

Dodoma is a city in Tanzania

The child is drawing a circle

Ee



a e i o u

Ee-Embe-Shangazi yangu anakula embe

Ee-Elimu-Elimu ni mali

Ee-Endesha-Endesha gari polepole

Ee-Endelea-Endelea mpaka mwisho

Ee-Eneo-Eneo hili ni kubwa

My aunt is eating a mango

Education is wealth

Drive the car slowly

Continue till the end

This area is big

Ff



fa fe fi fo fu

Fa-Familia-Familia yetu ina watoto wawili

Fe-Fenesi-Mimi ninapenda fenesi

Fi -Filimbi- Kaka anapiga filimbi

Fo-Fomu- Mama anajaza fomu ya shule

Fu-Funguo- Baba ana funguo mbili

Our family has two children

I like jackfruit

My brother is blowing a whistle

Mother is filling a school form

Dad has two keys

Gg



ga ge gi go gu

Ga-Gauni- Eva ana gauni jekundu

Ge-Geuka- Geuka nyuma

Gi- Giiza-Usiku kuna giza

Go-Goti-Goti langu linauma

Gu-Gunia- Mjomba wangu ana gunia la viazi

Eva has a red dress

Turn to your back

The night is dark

My knee is hurting

My uncle has a sack of potatoes

Hh



ha he hi ho hu

Ha-Harusi-Leo kuna harusi ya shangazi

He-Hereni-Hereni zangu ni ndefu

Hi- Historia-Nimesoma kitabu cha historia

Ho-Hoho-Mama anakula pilipili hoho

Hu-Huzuni- Kinyume cha huzuni ni furaha

Today is my aunt's wedding

My earrings are long

I read a history book

Mom is eating bell peppers

The opposite of sadness is happiness

li



a e i o u

li-Imba-Imba wimbo wa taifa
li-Ingia-Ingia ndani tucheze
li-Ita-Ita kwa sauti
li-Inzi-Inzi ni wachafu sana
li-Inama- Inama uvunguni uchukue viatu

*Sing the national anthem
Come in let's play
Call loudly
Flies are very dirty
Bend down and take shoes from under the bed*

Ji



ja je ji jo ju

Ja-Jani-Jani hili ni la kijani
Je-Jengo-Jengo la shule ni jeupe
Ji-Jicho-Jicho langu ni jeusi
Jo-Jogoo-Jogoo ana rangi ya kahawia
Ju-Jua-Jua lina rangi ya njano

*This leaf is green
The school bulding is white
My eye is black
The rooster has a brown color
The sun is yellow*

Kk



ka ke ki ko ku

Ka- Kalamu-Dada ana kalamu nyekundu

Ke-Kengele-Shule ina kengele nyeupe

Ki-Kichwa- Samaki ana kichwa cheusi

Ko-Kochi-Mimi nina kochi la bluu

Ku-Kuku-Kuku ana rangi nyeupe

My sister has a red pen

The school has a white bell

The fish has a black head

I have a blue couch

The chicken has a white color

Ll



la le li lo lu

La-Lala-Lala mapema usichelewe kuamka

Le-Leo-Leo ni siku gani?

Li- Limao-Mjomba anakula limao

Lo-Lori- Lori lina tairi nyeusi

Lu-Lulu-Wewe ni lulu ya taifa

Sleep early so that you don't wake up late

What day is it?

Uncle is eating a lemon

The truck has black tyres

You are a treasure to the nation

Mm



ma me mi mo mu

Ma-Matango- Mimi napenda kula matango

Me-Meza-Meza ya mwalimu ni nyeusi

Mi-Miti-Shamba lina miti miwili

Mo-Moja-Mimi nina simu moja

Mu-Mungu-Mungu amejaa upendo

I love to eat cucumbers

The teacher's table is black

The farm has two trees

I have one phone

God is full of love

Nn



na ne ni no nu

Na-Nanasi- Babu anakula nanasi moja

Ne-Neti- Baba ana neti mbili za mbu

Ni- Ni-Mimi ni mtoto mdogo

No-Noeli-Leo ni sikukuu ya Noeli

Nu-Nusu-Weka maji nusu kikombe tafadhali

Grandpa is eating one pineapple

Dad has two mosquito nets

I am a young child

Today is Christmas day

Put half a cup of water please

Oo



a e i o u

- Oo-Ogelea-Ogelea polepole!
- Oo-Ongea-Ongea kwa sauti tafadhali.
- Oo-Osha-Osha gari vizuri
- Oo-Ona-Ona! Mama amenipa zawadi nzuri
- Oo-Onja-Onja chakula changu kitamu

Swim slowly

Speak loudly please

Wash your car properly

Look!My mother gave me a nice gift

Taste my yummy food

Pp



pa pe pi po pu

- Pa-Papai-Mjomba anakula papai
- Pe-Penseli-Mimi nina penseli tatu
- Pi- Pipi-Naomba pipi kijiti tafadhali
- Po-Popo-Popo huwa analala mchana
- Pu-Pua-Pua yangu inauma

Uncle is eating papaya

I have three pencils

Can I have a lollipop please?

Bats sleep during the day

My nose is hurting

Rr



ra re ri ro ru

Ra-Ramani-Hii ni ramani ya Tanzania
Re-Reli-Baba anajenga reli
Ri-Risiti -Muuzaji amenipa risiti
Ro-Roho-Mama yangu ana roho nzuri
Ru-Ruka-Ruka juu zaidi

*This is a Tanzanian map
Dad is constructing a railway
The shopkeeper gave me a receipt
My mother is very kind
Jump higher*

Ss



sa se si so su

Sa-Samaki-Babu anapenda samaki
Se-Sema-Siku zote sema ukweli
Si-Simu-Simu ya mama inaita
So-Soma-Soma kwa bidii mwanangu
Su-Suti-Baba amevaa suti nyeusi

*Grandpa likes fish
You should always tell the truth
Mom's phone is ringing
Study hard my child
Dad is wearing a black suit*

Tt



ta te ti to tu

Ta-Taa-Taa hii ina mwanga mkali
Te-Tenesi-Kaka ana vi-tenesi vinne
Ti- Timu-Tanzania ina timu tano
To-Tofali- Tunatumia tofali kujenga nyumba
Tu-Tuzo-Dada yangu ameshinda tuzo sita

*This light is very bright
Brother has four tennis balls
Tanzania has five teams
We use bricks to build the house
My sister has won six awards*

Uu



a e i o u

Uu-Uyoga-Leo nimekula uyoga
Uu-Ukuta-Ukuta wa shule ni mrefu
Uu-Uji-Mimi ninapenda uji
Uu-Uzi-Mama ana uzi mweusi
Uu-Ugali-Leo tumepika ugali

*Today I ate mushroom
The school wall is long
I love porridge
Mom has a black thread
Today we cooked ugali*

Vv



va ve vi vo vu

Va-Vazi-Mtoto amevaa vazi la kiafrika

Ve-Veranda-Baba amekaa kwenye veranda

Vi- Vijiko-Mama ana vijiko saba

Vo-Volkano-Kilimanjaro ni mlima wa volkano

Vu-Vumbi-Kijijini kwetu kuna vumbi jekundu

The child is wearing an african attire

Dad is sitting at the balcony

Mom has seven spoons

Kilimanjaro is a volcanic mountain

Our village has red dust

Ww



wa we wi wo wu

Wa-Wali-Wali maharage ni mtamu!

We-Wembe-Wembe ni mkali sana

Wi- Wigi-Mama amevaa wigi

Wo-Wote-Watoto wote wamevaa sare

Wu-Wuwu-Mbwa anabweka “wu,wu,wu”

Rice and beans is yummy

The razor is very sharp

Mom is wearing a wig

All the kids are in uniform

The dog is barking “woof, woof, woof”

Yy



ya ye yi yu yu

Ya-Yai-Yai la kuku ni jeupe

Ye-Yeye-Yeye ni binamu yangu

Yi- Yiana ni msichana mrembo

Yo-Yote- Mama alikula asali yote

Yu-Yule-Mtoto yule ana vitabu kumi

The chicken egg is white

She is my cousin

Yiana is a beautiful girl

Mom ate all the honey

That kid has ten books

Zz



za ze zi zo zu

Za-Zabibu-Mtoto anakula zabibu

Ze-Zetu-Meza zetu zimevunjika

Zi- Zizi-Zizi la ng'ombe ni kubwa

Zo-Zoezi-Mimi napenda zoezi la kuhesabu

Zu-Zulia-Shangazi yangu ana zulia jekundu

The kid is eating grapes

Our tables are broken

The cow barn is big

I like a counting exercise

My aunt has a red carpet

Pronunciation Tip for Non-Swahili Speakers

Swahili has five vowels: a, e, i, o, u. the vowels are pronounced as follows:

A - ah (Like the "a" in "father")

E - eh (Like the "e" in "egg")

I - ee (Like the "ee" in "bee")

O - oh (Like the "o" in "pot")

U - oo (Like the "oo" in "book")

Tips for Non-Swahili Speakers

The Swahili alphabet consists of:

Vowels (Refer to module 1 of Swahili Strong Foundation): Aa, Ee, Ii, Oo, Uu.

Consonants: b, ch, d, f, g, h, j, k, l, m, n, p, r, s, t, v, w, y, z.

What's different from the English alphabet?

Notice the 'H' added to the C? Swahili doesn't have a c consonant in Swahili. It's Ch.

X and Q are not included in the Swahili alphabet.

In Swahili we do not pronounce plain consonants , it has to go with a vowel eg b=be . Therefore the alphabet is pronounced as follows:

A, be, che de, e, Fe, ge, I, je, ke, le, Me, ne, o, pe, re, Se, te, u, ve, we, ye, ze.

Simplified way to pronounce vowels and consonants

A, e, i, o, u

Ba, be, bi, bo, bu

Cha, che, chi, cho, chu

Da, de, di, do, du

Fa, fe, fi, fo, fu

Ga, ge, gi, go, gu

Ha, he, hi, ho, hu

Ja, je, ji, jo, ju

Ka, ke, ki, ko, ku

La, le, li, lo, lu

Ma, me, mi, mo, mu

Na, ne, ni, no, nu

Pa, pe, pi, po, pu

Ra, re, ri, ro, ru

Sa, se, si, so, su

Ta, te, ti, to, tu

Va, ve, vi, vo, vu

Wa, we, wi, wo, wu

Ya, ye, yi, yo, yu

Za, ze, zi, zo, zu

Other Swahili Letter Combinations include:

Bw = bwa bwe bwi bwo bwu	eg:	Bwana (sir)
Dh = dha dhe dhi dho dhu	eg:	Dhahabu (gold)
Gh = gha ghe ghi gho ghu	eg:	Ghali (expensive)
Gw = gwa gwe gwi gwo gwu	eg:	Gwiji (expert)
Kh = kha khe khi kho khu	eg:	Khanga (cloth)
Kw = kwa kwe kwi kwo kwu	eg:	Kweli (true)
Mb = mba mbe mbi mbo mbu	eg:	Mbali (far)
Mv = mva mve mvi mvo mvu	eg:	Mvua (rain)
Mw = mwa mwe mwi mwo mwu	eg:	Mwalimu (teacher)
Nd = nda nde ndi ndo ndu	eg:	Ndizi (banana)
Ng = Nga nge ngi ngo ngu	eg:	Ngazi (stairs)
Ng' = ng'a ng'e ng'i ng'o ng'u	eg:	Ng'ombe (cow)
Nj = nja nje nji njo nju	eg:	Njaa (hunger)
Ny = nya nye nyi nyo nyu	eg:	Nyama (meat)
Nz = nza nze nzi nzo nzu	eg:	Nzuri (nice)
Pw = pwa pwe pwi pwo pwu	eg:	Pweza (octopus)
Sh = sha she shi sho shu	eg:	Shule (school)
Sw = swa swe swi swo swu	eg:	Swali (question)
Vy = vya vye vyi vyo vyu	eg:	Vyombo (utensils)
Th = tha the thi tho thu	eg:	Thanmani (value)
Chw = chwa chwe chwi chwo chwu	eg:	Kichwa (head)
Mbw = mbwa mbwe mbwi mbwo mbwu	eg:	Mbwa (dog)
Nyw = nywa nywe nywi nywo nywu	eg:	Nywele (hair)

Koᅇa ya Mzazi/Mwalimu

Kupitia kitabu hiki mwanafunzi anajenga msingi bora katika kutamka, kuandika na kusoma kiswahili. Kitabu hiki kinaweka msisitizo kwenye silabi (Mfano ba be bi bo bu) ili kurahisisha matamshi ya maneno.

Pamoja na kujifunza herufi zote ndani ya alfabeti na silabi zake, kitabu hiki pia kinafundisha juu ya namba; (moja mpaka kumi); rangi; misamiati kuhusu wanafamilia (baba, mama, shangazi, mjomba, kaka, dada, binamu); Vitenzi (Kupenda, kupika, kula, kulala, kuona, kuwa, kuwa na, kwenda, nk); Mchanganyiko wa silabi, maneno na sentensi fupi unamwandaa mtoto kuweza kumudu mazungumzo ya kawaida katika mazingira yanayomzunguka.

Teacher/Parent Corner

Through this book, the student builds a strong foundation in pronouncing, writing and reading in Swahili. This book puts emphasis in syllables (eg ba be bi bo bu) to allow easy pronunciation of words.

This book not only teaches all the letters and their syllables, but also about Numbers(one to ten); Colours; vocabularies about Family (mom, dad, aunt, uncle, brother, sister, cousin); Nouns(eat, cook, sleep, see, go etc). The combination of syllables, words and short sentences prepares the student to be able to navigate everyday conversations in their immediate surroundings.

Koŋa ya Mzazi/Mwalimu

Kama mzazi/mwalimu, unaweza kutumia vidokezo vifuatavyo kumjengea mwanafunzi msingi bora:

-Mtamkie mtoto silabi moja moja, maneno na sentensi fupi

-Mpe mwanafunzi zoezi la kuandika alfabeti kuanzia a-z na silabi zake kwa kufuata utaratibu wa a e i o u, ba be bi bo bu.

-Jadili na mwanafunzi ili kumpa motisha wa kutamka alfabeti ili kumjengea uwezo wa kusoma na kuongea

-Mpe mwanafunzi changamoto ya kutengeneza neno moja kwa kila herufi na kulitungia sentensi fupi.

-Mpe mwanafunzi zoezi la kuchora vitu vinavyoendana na herufi zote.

Teacher/Parent Corner

As a parent or teacher, you can use the following tips to help build a strong foundation for the student:

-Read to your student each syllable, words and short sentences.

-Give the student an assignment to write the alphabets from A-Z together with the syllables using the order of a, e, i, o, u and ba,be,bi,bo,bu

-Conversate with the student in order to give them motivation in pronouncing the alphabets and syllables to give them a good reading and speaking foundation.

-Challenge the student to make a word for each letter and use it in a sentence.

-Ask the student to draw an object that corresponds to each letter.

Would you like to receive more kid-friendly Swahili learning resources? Sign up on the link below to be added to our mailing list:

<https://mailchi.mp/9846d677d62a/swahilihome>

Your feedback is important to us. To help us improve our future offerings please share your child/students' experience with this resources by contacting:

KiswahiliOttawa@gmail.com